YALIYOMO

Tanzania tunayoitaka 1

Utangulizi 7

Elimu 9

Afya 11

Kilimo 13

Uchumi 15

Michezo 18

Utawala Bora 19

Mapendekezo ya Mfumo Mpya wa Utawala. 22



TANZANIA TUNAYOITAKA

Ndugu zangu Watanzania

Tangu Tanzania ilipopata Uhuru yapata miaka 44 sasa bado haijapiga hatua kubwa katika maendeleo ya wananchi wake. Katika sehemu nyingine zimepiga hatua kurudi nyuma. Kwa mfano pato la Mtanzania limezidi kushuka ambapo liko chini ya dola moja kwa siku ikilinganisha na dola 4 miaka ya sabini. Tanzania impeata sifa ya kuongoza katika umaskini wa kutupwa na utegemezi. Sababu nyingi zinazotolewa na Utawala wa CCM ni za kubuni na hazina mantiki yoyote kwa mfano vita vya Iddi Amin, mafuriko na Ukame.

CHADEMA hairidhiki hata kidogo na sababu hizi. Baada ya kutafakari hali hii kwa kina, CHADEMA imeng'amua kuwa chanzo na kiini cha Umaskini wetu uliokithiri na kudorora kwa maendeleo ni **mfumo mbovu** wa Utawala. Kwa hiyo CHADEMA inasema kwamba ili Maenendeleo ya kweli na ya kudumu yapatikane ni lazima kuwepo mabadiliko ya kweli na uhuru awa kweli katika mfumo wa Utawala.

Wakati akihutubia Umoja wa Mataifa mwaka 1958, Mwalimu Julius Nyerere alisema, Tunapodai Uhuru kutoka kwa Waingereza sio kwamba tunataka waingereza watupe Utawala tu, bali waingereza wameshindwa kuondoa Umaskini, Waingereza wameshindwa kuelimisha Watanganyika na pia wameshindwa kutoa huduma za Afya. Tunadai ili kupigana na maadui watatu – Ujinga, Umaskini na Maradhi.

CHADEMA tunakubaliana na maneno ya Mwalimu kwani Uhuru wa kweli ni Uhuru unaoboresha maisha ya watu. Hata hivyo Watanzania hawajafaidi Mtunda ya Uhuru wa kweli kwa kuwa ujinga umeongezeka, maradhi yanatumaliza na ufukara umekithiri. Ni miaka 44 sasa tangu tupate uhuru lakini bado Watanzania tunaishi maisha duni sana. Hii imetokana na Uongozi mbovu na mfumo mbovu wa awamu zote tatu za Utawala wa Serikali ya CCM.

Akizungumzia suala la Maendeleo, Mwalimu pia aliwahi kusema "Ili tuendelee tunahitaji vitu vinne, Watu, Ardhi, Siasa safi na Uongozi bora. Mipango mingi chini ya Serikali ya CCM imeshindwa kutekeleza matakwa ya kauli hizo za Mwalimu.

Ili kuondokana na hali hii CHADEMA Chama Mbadala kimedhamiria kuleta mabadiliko ya kweli na Uhuru wa Kweli. Uhuru utakaowawezesha Watanzania kujikomboa kwa kuboresga Elimu, kufufua Kilimo, kuongeza Ajira, Afya wote na kukomesha Rushwa.

CHADEMA imeonesha kwa vitendo kwamba mipango yake ya Maendeleo inatekelezeka. Haya yamedhihirika katika Halmashauri zinazoongozwa na **CHADEMA** za **Kigoma Ujiji**, **Karatu na Hai**. Ndani ya miaka mitano katika kuongoza Halmashauri hizi tumeweza kuleta mabadiliko makubwa katika kuboresha hali za wananchi. Hii ni pamoja na kufuta kodi na kuboresha huduma za jamii kama maji na elimu ya Sekondari. Kufuatia Sera yetu ya kufuta kodi za Manyanyaso kwa wananchi Serikali ya CCM iliiga na kufuta kodi nchi nzima. Mafanikio haya makubwa yamepatikana licha ya uwezo na mizengwe mingi inayowekwa na Utawala wa CCM.

CHADEMA inatambua uwezo wa wananchi katika kujiletea maendeleo yao wenyewe. Hivyo, Serikali ya CHADEMA itawajengea mazingira mazuri wananchi ili kuweza kuendesha shughuli zao bila kubughudhiwa kwa kujenga ubunifu na ujasiriamali; Sera sahihi na kuwawezesha wananchi kufurahia matunda ya Uhuru na maendeleo. Hivyo **CHADEMA** imepanga safu zake tayari kabisa kushinda na kuendesha Serikali inayowajibika na kuwajali watu wake.

Mimi kama kiongozi Mkuu wa **CHADEMA**, nitasimamia mabadiliko ya kweli na uhuru wa kweli kuunda Taifa la watu walio huru na lenye kuzingatia misingi ya Utawala bora na linalotoa fursa kwa wananchi wake kushiriki katika kuboresha maisha yao. Tanzania endelevu, yenye haki na isiyovumilia ukandamizaji wa aina yeyote kwa wananchi wake – ndiyo Tanzania tunayoitaka.

Nitahahakisha kwamba vyombo vya Utawala vitakavyoundwa na Viongozi wa **CHADEMA** mtakaowachagua – Rais, Wabunge, wawakilishi na Madiwani wanafanya maamuzi ya busara na makini yatakayowaletea wananchi nafuu ya maisha na kuwapa matumaini ya kuendelea na kupiga hatua za kimaisha katika Nyanja zote za maendeleo.

Ilani hii ya uchaguzi inazungumzia mikakati halisi kama CHADEMA itashinda Uchaguzi na kuongoza dola. Vilevile ilani hii ndio itakayokuwa rejea yetu katika michango ya wabunge wa **CHADEMA** katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika Ilani hii tumegusia masuala machache ambayo **CHADEMA** inadhani ni muhimu sana katika kurudisha Tanzania katika njia ya maendeleo. Haya ndiyo wanaCHADEMA tunayoyaamini na kwamba yakifanyiwa kazi katika miaka mitano ijayo tutajenga misingi ya kweli ya Taifa la Watanzania walio huru, wasio waoga, wenye fursa ya kuboresha maendeleo yao.

Kama nilivyoeleza hapo juu, **CHADEMA** tumeonyesha kwa vitendo uadilifu wetu katika kutekeleza ahadi tunazozitoa kwa wananchi, Kama wananchi walivyotuamini **Hai, Karatu na Kigoma Ujiji**, tunaomba wananchi mtuamini ili tuweze kusambaza mafanikiko haya katika Nchi nzima. Tarehe

30 Oktoba tunakuomba ujitokeze uwapigie kura Mgombea Urais wa **CHADEMA**, Mgombea Ubunge wa **CHADEMA** Mgombea Uwakilishi wa **CHADEMA** na Mgombea Udiwani wa **CHADEMA** kama Watanzania tunataka maendeleo ya kweli na ya kudumu hatuna budi kuwakataa Viongozi walaghai wanaoibukia kila wakati wa Uchaguzi wakiwarubuni wapiga kura na ahadi lukuki zisizotekelezeka. Watanzania lazima tuelewe kwamba mabadiliko ya kweli yataletwa kwa kubadilisha mfumo mzima wa Utawala na kuweka Viongozi wapya. **Maendeleo ya kweli hayawezi kuletwa na Mafisadi walewale wa Chama kilekile chenye uozo uleule wakiendeleza yaleyale kwa kasi Mpya, Nguvu Mpya na Ari mpya. CHADEMA inaamini kwamba kwa falsafa ya Chukua Chako Mapema (CCM), Tanzania yenye neema kamwe haitawezekana.**

KWA NGUVU YA UMMA TUTASHINDA!

CHADEMA: Mbadiliko ya kweli, Uhuru wa kweli, Maendeleo ya kweli.

Asanteni sana.

UTANGULIZI

Mojawapo ya vigezo vya Utawala mbaya ni sera mbovu. Kwa muda mrefu sasa Tanzania imepita katika vipindi tofauti vyenye mielekeo na sera tofauti. Kuanzia mwaka 1967 hadi 1987 tukiwa chini ya Utawala wa Chama kimoja, Tanzania ilikumbatia itikadi ya Ujamaa na kujitegemea. Mpaka sasa ni dhahiri kwamba itikadi hii imeachwa na wenyewe wa CCM ingawaje bado imebakizwa kwenye katiba na katika maneno ya baadhi ya Viongozi. Hii ina maana kwamba CCM haijawa na mwelekeo ulio wazi.

Mazoea ya Utawala katika Ilani na program za Chama chao ni kuorodhesha kila kitu bila kuweka kipaumbele au kuchanganua jinsi maeneo tofauti yanavyotegemeana katika kusukuma maendeleo kwa Ujumla. Ni kawaida mfano kwa ilani za CCM kuorodhesha Kilimo, Ufugaji, Viwanda, elimu, afya n.k bila kuweka uzito na kuonyesha ni kipi kitangulie. Utekelezaji wake umekuwa ni wa ubabaishaji kwa kuwa unagusa kila eneo ili mradi ionekane machoni pa wananchi kuwa mambo yamefanyika katika kila eneo. Matokeo ni kwamba hakuna hata kimoja kinachofanyika kwa ufanisi na maeneo mengine muhimu kama kilimo hutekelezwa, Maendeleo kudidimia na Umasikini kukithiri hasa miongoni mwa wakulima.

Ili kuleta mabadiliko ya kweli katika suala la sera na utekelezaji wake, **CHADEMA** imeazimia kufanya mabadiliko ya kweli ili kuleta Uhuru na maendeleo ya kweli katika maeneo Makuu matano nayo ni Elimu, Kilimo,

Afya Ajira na mfumo mpya wa Utawala. Katika kuhakikisha kuwa sera hizi zinatekelezeka, **CHADEMA** itafanya yafuatayo.

- Kupambanisha maeneo machache muhimu ambayo kwa pamoja yatachangia kutoa chachu ya kufufua uchumi na Maendeelo ya jamii.
- Kutambua sekta Uongozi na kuipa kipaumbele maalum ili iweze kuyasukuma maeneo mengine. Hii ni sekta ya elimu.
- Kuchanganua na kueleza umuhimu wa maeneo hayo na yanavyoungana ili kuongeza tija na ufanisi kuleta Maendeleo.

1. ELIMU

HALI HALISI YA ELIMU TANZANIA IKOJE?

Ubora wa Elimu Tanzania umeporomika:-

Wanafunzi wanarundikana madarasani na wengine hata kusomea chini ya miti, Mtaala haienani na hali halisi, vipaji haviendelezwi. Mazingira ya shule hayana mtazamo wa kijinsia na hayawajali watoto wenye ulemavu. Mfumo wa elimu ya msingi haumwandai mwanafunzi kuwa Raia wa kujitegemea anapohitimu.

Bajeti ya Elimu Finyu.

Waalimu ni wachache, wamefukarishwa na hawaendelezwi kitaaluma, shule na vyuo hazina vifaa vya kuweza kutosheleza ongezeko la wanafunzi.

Gharama za Elimu bado ni mzigo mkubwa kwa familia Maskini.

Wazazi wengi wameshindwa kupeleka watoto wao katika shule za Sekondari na vyuo vya Elimu ya juu ilhali walionacho wachache wanasomesha watoto wao katika shule za gharama kubwa. Matokeo yake mfumo wa elimu unajenga matabaka ya matajiri walioelimika na Maskini mbumbumbu.

SERIKALI YA CHADEMA ITAFANYA NINI?

CHADEMA inaamini kwamba elimu ndio chimbuko la maendeleo ya binadamu yeyote yule. Tunatambua kwamba mataifa yaliyoendelea mengine yakiwa ni machanga kama Tanzania yamezingatia kuwekeza katika Elimu. Kwa CHADEMA elimu ndio sekta Uongozi katika kuchojea maendeleo, Mabadiliko na Uhuru wa kweli, kwa lengo hili basi, **CHADEMA** inaboresha elimu kwa kuipa kipaumbele.

Itabadili mitaala ya elimu.

Mitaala italenga mahitaji na maslahi ya Taifa, na kuchochea fikra, udadisi, ugunduzi na kuendeleza vipaji. Masomo ya biashara na kilimo yatarejeshwa katika mitaala. Mashindano ya Umiseta na Umitashumta yatarejeshwa. Elimu ya awali mpaka kidato cha pili itakuwa ya lazima na bure kwa kila Mtanzania.

Bajeti ya elimu kupanda kutoka 9% mpaka 35%

Itajali waalimu kwa kuboresha kipato, makazi na mafunzo yao. Shule na vyuo vitapatiwa vifaa vya kiada na ziada vya kutosha.

Itapunguza mzigo wa gharama za elimu kwa watanzania maskini

Itatoa ruzuku kwa shule za Sekondari na vyuo vya elimu ya juu, Itabadili shule za Serikali kuwa ni vituo vya Ubora wa elimu ili kuondoa matabaka.

1. AFYA

HALI HALISI YA AFYA TANZANIA IKOJE?

Gharama za afya ni mzigo kwa wananchi;

Serikali imekwepa jukumu la kutoa huduma za afya kwa wananchi Huduma za afya zimekuwa za kibiashara.

Huduma ya afya haziridhishi,

Licha ya kuchangia gharama huduma ni mbaya na zinatolewa kwa misingi ya rushwa. Wakati wananchi wanapoteza maisha yao kwa magonjwa yanayotibika kama Malaria Viongozi wanafuja fedha nyingi za Umma kutibiwa nje ya Nchi. Inasikitisha zaidi kuona kina mama wajawazito wakililazimishwa kwenda kujifungua na vifaa kama vile Pamba, gloves na hata nyembe! Hii imefanya kina mama waendelee kujifungulia majumbani au hata kwa wakunga wa jadi kwa kukosa vifaa husika. Kujifungua ni jambo linalostahili staha na faragha.

Madaktari na Manesi wanapata maslahi duni, Vitendea kazi haba na chakavu na Hospitali chafu. Hali hii imewajengea wahudumu wa afya mazingira ya rushwa.

SERIKALI YA CHADEMA ITAFANYA NINI?

CHADEMA inaamini, kuwa afya bora ndio msingi wa maendeleo. Wananchi wasio na afya bora hawataweza kujishugulisha katika ujenzi wa Taifa leo na

katika kujipatia kipato cha kuendesha maisha yao ya kila siku. Tunatambua kuwa Mataifa mengi yaliyoendelea yamefanikiwa kwa kuwekeza katika afya. Kwa CHADEMA sekta ya afya itaboreshwa zaidi ili wananchi wote waweze kupata huduma hii muhimu ili waweze kuchangia vyema katika maendeleo ya nchi yao.

Gharama nafuu za huduma ya afya.

Itapanua mpango wa bima ya afya kwa kumshirikisha kila Mtanzania. Huduma zote zinazohusu afya ya mama na mtoto zitaondolewa kodi na kutengewa fedha za kutosha. Itatoa tiba ya malaria bure.

Huduma kwa wanaoishi na VVU,

Serikali za mitaa zitawahudumia watu wanaoishi na VVU kwakuwapatia dawa za kurefusha maisha na mafunzo ikiwemo lishe bora.

Bajeti ya afya kuongezwa.

Maslahi na vitendea kazi vya Madaktari na Manesi kuboreshwa. Itatoa motisha kwa Hospital safi.

2. KILIMO

Kilimo kimedorora,

Licha ya KILIMO kuchangia asilimia 44% ya pato la Taifa wananchi bado wanategemea jembe la mkono na mvua zisizotabirika. Barabara hazifiki vijijini na hivyo mazao kuoza kabla ya kufika sokoni.

Soko linalonyonya wakulima,

Wachuuzi wanadhulumu wakulima kwa kununua mazao kwa bei ya kutupa. Sera potofu za soko holela zimeua kabisa motisha wa kulima.

Tunauza mazao ghafi.

Hakuna viwanda vidogo vya kuhifadhi na kusindika mazao ya kilimo.

CHADEMA ITAFANYA NINI?

CHADEMA inatambua umuhimu wa kilimo katika maisha ya mtanzania Asilimia 80 ya watanzani wanategemea kilimo. Tanzania ilikua ni nchi pekee katika afrika iliyokuwa na kiwango kikubwa cha uzalishaji wa mazao ya chakula katika miaka ya sitini na sabini. Hivi sasa Tanzania inategemea misaada ya vyakula kutoka nje na uingizaji wa vyakula umekuwa ukiongezeka kila siku. Hii ni aibu kwa nchi yetu iliyo na vyanzo vingi vya

maji kama vile mito na maziwa. Kilimo cha umwagiliaji kitapewa kipaumbele.

Itatafuta kodi,

Kodi zote za pembejeo za kilimo ikiwemo VAT zitaondolewa. Itatoa ruzuku kwa wakulima wetu. Itaanza kilimo kikubwa cha umwagiliaji maji.

Soko la Mazao

Soko holela itadhibitiwa. Itaweka kipaumbele kujenga miundo mbinu ya barabara ziendazo vijijini. Itatoa motisha na usahuri kwa wakulima kuzalisha mazao mbadala ya biashara kama maua, viungo na mboga.

Usindikaji,

Itatoa ruzuku na motisha kwa uzalishaji wa chakula na usindikaji wa mazao ya kilimo. Itahamasisha wakulima kuuza bidhaa zilizoongezwa thamani.

4. UCHUMI

NINI HALI HALISI YA UCHUMI TANZANIA?

Uchumi unamilikiwa na wageni na mataraji wachache.

Ukuaji wa uchumi haujanufaisha wananchi walio wengi. Tofauti ya wenye kipato na wasio nacho inazidi kuwa kubwa. Kati ya Watanzania 100 ni 44 tu wana uhakika wa mlo mmoja kwa siku.

Ajira hakuna

Watanzania wengi hasa vijana wanaishi maisha ya kubangaiza kwa kukosa kazi. Wageni wanaajiri wageni wenzao na watoto wa vigogo. Hata Watanzania wachache waliobahatika kuajriwa na wawekezaji wa nje wanalipwa maslahi duni kulinganishwa na wageni.

Mzigo wa Kodi,

Kodi ni kubwa, nyingi za kificho na hazilipiki. Wageni wanapewa misamaha ya kodi kiholela, kwa upendeleo na katika mazingira ya rushwa.

SERIKALI YA CHADEMA ITAIMARISHA UCHUMI.

CHADEMA inaamini kuwa uchumi katika nchi yoyote ile ndio chimbuko la Maendeleo. Uchumi unapokuwa mzuri na nchi imekuwa na maendeleo. Hii ni kusema kuwa uchumi ndio kipimo cha maendeleo ya nchi. Inasikitisha

sana kuona Tanzania pamoja na utajiri wote ilio nao, bado Uchumi wetu uko chini mno. Katika nchi 208 duniani Tanzania ni nchi ya 206 kwa umasikini (World Economic Report 2004). **CHADEMA** itaimarisha uchumi kwa kuboresha sekta zote ili ziweze kuliingiza Taifa fedha za kigeni kama vile sekta za Madini, Utalii, Kilimo, Viwanda n.k

CHADEMA inaamini kuwa wanawake wamekuwa wakichangia uchumi wa nchi hii kwa kiasi kikubwa. Vilevile historia imethibitisha kuwa mfumo dume katika nchi nyingi za Afrika umekuwa ukiwakandamiza na kuwanyanyasa wanawake katika kila sekta zikiwemo za elimu, ajira na hata zile za ustawi wa jamii. Ni katika mazingira haya basi **CHADEMA** imeona haja ya kuboresha maisha ya wanawake kwa kuwawezesha waweze kujiletea maendeleo yao. Hii ni pamoja na kuwaendeleza kielimu, kuwapatia mikopo na kuhakikisha kuwa kuna usawa katika ngazi zote za Utawala.

CHADEMA itatunga na kutekeleza sera zinazojali watu maskini-:

Itawezesha watanzania wanawake kwa wanaume kumiliki uchumi wao wenyewe. Itawezesha kila Mtanzania kumiliki mali bila mizengwe ikiwemo mali za vipaji.

Kodi zinazotozwa zitawekwa wazi.

Itapunguza VAT mpaka 16%. Tutaziba mianya ya ukwepaji kodi na kutoa misamaha ya kodi pale tu inapobidi na lazima iidhinishwe na Bunge. Itafuta kodi zote za huduma na bidhaa za akina mama wajawazito na watoto.

Itaongeza ajira-:

Itatengeneza ajira kuimarisha sekta za ujenzi, madini, kilimo, utalii na huduma za jamii. Itaweka kipaumbele kwa sekta za uchumi zinazotengeneza ajira kwa watu wengi mfano kilimo. Kwa kuwa kipaumbele kimewekwa kwenye elimu. **CHADEMA** kinaamini kuwa shule nyingi zaidi zitajengwa. Kwa hivyo basi waalimu zaidi wataajiriwa. Vilevile, ajira nyingine zitatokana na sekta binafsi. Wananchi wengi hasa vijana watajengewa mazingira mazuri kwa kupewa mikopo kwa ajili ya kuanzisha miradi mbalimbali. Itatoa leseni za bure na likizo ya kodi kwa vijana wafanyabiashara ndogondogo na vijana wanaojishughulisha na uzalishaji mali.

5. MICHEZO

CHADEMA inaamini kuwa michezo ni muhimu sana kwa afya lakini pia inaleta sifa kwa Taifa, kwa mfano Tanzania ilifahamika sana mwaka 1976 wakati **Filbert Bayi** alipotwaa medali ya dhahabu; kabla ya **Simba** Ilipofikia

fainali za klabu bingwa ya Afrika. **CHADEMA** tunajiuliza mafanikio hayo yameenda wapi? Kuna tatizo gani?

Michezo itawapatia vijana ajira. CHADEMA itawaandaa watoto na vijana wadogo (yoso chini ya miaka 15) wenye vipaji vya kucheza kandanda na riadha kwa ajili ya kuunda kikosi cha Taifa kwa kipindi cha zaidi ya miaka mitano. Vijana hawa watapangiwa vituo maalum, mafunzo maalum na chakula maalum, Pia kutakuwapo na chombo cha kandanda ambacho kitakuwa na mtandao nchi nzima na kushirikisha wanamichezo kuanzia ngazi ya vijiji na kujumuisha Taasisi mbalimbali kama vile shule na makundi mbalimbali ya kijamii.

6. UTAWALA BORA

HALI HALISI IKOJE?

Kuna ubadhilifu mkubwa wa mali za umma kutokana na rushwa na Ufisadi:

Kila mwaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali anatoa taarifa Bungeni akionyesha fedha nyingi ambazo zimepotea na hazina maelezo ya kutosha kwenye Wizara na Idara za Serikali. Ubinafsishaji holela wa Mashirika ya Umma. Viongozi wa CCM wamejitwalia nyumba na mali za Umma.

Uonevu na Unyanyasi wa Raia.

Uonevu wa wazi wa vyombo vya dola kama polisi kwa wananchi wasio na hatia. Watendaji wa vijiji na kata (VEO na WEO) wananyanyasa wananchi na wanajifanya miungu watu.

Mwingiliano kati ya Serikali Kuu na Mitaa.

Serikali kuu inaingilia Serikali za Mitaa. Katiba haiku wazi juu ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Wakuu wa wilaya wanaingilia Halmashauri za Wilaya na kudhoofisha Demokrasia.

Mfumo wa Muungano una kasoro.

Watanzania hawajapata fursa ya kujadili mfumo wa Muungano wanaoutaka uwe namna gani.

CHADEMA ITABADILI MFUMO WA UTAWALA.

CHADEMA inaamini kuwa mfumo mbaya wa Utawala wa CCM umechangia kwa kiasi kikubwa hali mbaya ya rushwa na Ufisadi uliopo nchini. Kadri siku zinavyosonga mbele ndivyo hivyo hali ya rushwa na kukaa tama kwa wananchi inavyozidi. CCM ikaona ibadili rushwa na kuliita takrima ili kuendeleza ufisadi wao. Viongozi wengi wamekuwa ni wa kuteuliwa na Rais

na sio wa kuchaguliwa na wananchi. Hali hii imewafanya wananchi wasiwe na imani na Viongozi hao kwani badala ya Viongozi kuwajibika kwa wananchi, wananchi wamekuwa wakiwajibika kwa Viongozi.

CHADEMA itabadili mfumo wa Utawala kwa kuhakikisha kuwa Viongozi wote wanachaguliwa na wananchi ili wawajibikaji kwa wananchi. Vyeo vya Ukuu wa Wilaya na Mikoa vitafutwa. Badala yake Mabarza ya Kanda na Halmashauri za Wilaya na Manispaa zitasimamia shughuli zote za utendaji. Wananchi kuchagua Meya au Wenyeviti wa Halmashauri. Mikoa itapunguzwa na itaitwa majimbo yatakayokuwa kumi. Itaimarisha Serikali ya Kijiji kama chombo cha msingi cha Uongozi.

Itahahakisha Utawala bora.

Itarejesha nyumba za Serikali walizojiuzia Viongozi. Itarejesha Serikalini mali zote zilizohodhiwa na CCM kama viwanja vya mpira, maegesho ya magari na majengo.

Itavunja PCB na kufanya rushwa kuwa kosa la jinai chini ya Mkurugenzi wa makosa ya jinai.

Itawezesha wananchi kuandika katiba mpya mapema iwezekanavyo. Madiwani na wabunge kuwajibishwa na wananchi kwa mujibu wa Katiba.

CHADEMA itaheshimu haki za binadamu.

Itawapatia polisi maslahi na mafunzo zadi ili waweze kusimamia kazi zao kwa haki. Itapiga marufuku VEO na WEO kutishia, kunyanyasa na kunyang’anya mali za wananchi.

CHADEMA itasimamia Muungano unaokubalika na pande zote.

MAPENDEKEZO YA MFUMO MPYA WA UTAWALA.



Mhe. Freeman aikaeli Mbowe

Mwenyekiti

UTEKELEZAJI WA SERIKALI YA CHADEMA NDANI YA MWAKA MMOJA TANGU KUINGIA MADARAKANI

1. ELIMU

Bajeti 2006/2007 kuongeza bajeti ya elimu kutoka 9% hadi 35% kuongeza ajira za waalimu.

2. AFYA

Bajeti ya 2006/2007

- Kutafuta VAT kwenye huduma na vifaa vya kina mama waja wazito na watoto.
- Madawa ya kurefusha masiha kw awatu wanaoishi na virusi vya Ukimwi kugawiwa kwa wote.
- Kupandisha Mishahara ya Madaktari na wauguzi.

3. KILIMO

- Bajeti 2006/2007 kutafuta kodi zote pamoja na VAT kwa pembejeo za Kilimo.
- Kuweka mpango thabiti w akutofautisha ardhi kwa ajili ya umwagiliaji.

4. UCHUMI

- Bajeti 2006/2007 kupunguza VAT kwa 16%
- Kufanya mapitio ya Mikataba yote ya uwekezaji na ubinfsishaji.
- Tanzania kujiunga upya na COMESA.
- Kutengeneza ajira Milioni moja kw akufanya mabadiliko makubwa katika Sekta za madini, Utalii, Ujenzi na huduma za jamii.
- Kuboresha maisha ya kinamama kwa kuwawezesha kielimu na kuwapa nafasi katika Utawala.

5. MFUMO NA UTAWALA BORA

Ndani ya miezi sita ya kwanza.

- Kurudisha Serikalini mali zote zilizochangwa na Wananchi na kuhodhiwa na CCM kama Viwanja vya Mpira na Majengo yanayotumiwa na CCM.
- Kurudisha nyumba zote za Seriklai walizojiuzia Viongozi.
- Kuanzisha Mchakato wa katiba mpya.
- Kuvunja PCB na kuweka majukumu yote ya kupambana na rushwa chini ya Mkurugenzi wa Makosa ya jinai (DCI).
-